

NI KOSA KUMWENDEA MUNGU ILI AKUPE MSAADA WAKATI

AKILINI MWAKO UMEPANGA/UNAJUA

NINI CHA KUFANYA.

MAANDIKO: 2WAFAL. 5: 1 – 14.

1. Utangulizi:

Katika biblia ipo mifano mingi ya watu waliotaka Mungu awafanyie mambo fulani fulani kama walivyopanga /wanavyotaka wao.

- Ndugu zangu, Mungu ana njia nyingi tofauti za kutufanyia mambo tofauti na akili zetu zinavyofikiri wakati wote.
- Hata mgonjwa huyu wa **Yoh. 5: 2 – 9** alikaa **miaka (38)** bila kupona, na Yesu alipofika pale alimuuliza swali jepesi tu **“wataka kuwa mzima”??** ona mlolongo wa majibu yake **“Yoh. 5: 7!!!** Kwa huruma tu Yesu aliona asipoteze muda kwa mgonjwa ambaye akilini mwake anangojea maji yatibuliwe na malaika na halafu awepo mtu wa kwanza kuingizwa ndani ya maji hayo na ndugu zake ili apone wa kwanza. Yesu akatoa amri **“ simama jitwike godoro lako,** uende na akapona saa hiyo hiyo. **Tusimpangie Mungu namna ya kufanya, njia zake ziko juu mno kuliko njia zetu na mawazo yake ni tofauti kabisa na mawazo yetu. Isay. 55:8 -9. Hili ndilo lilikuwa tatizo kubwa la Abrahamu kwanza. Mwanz. 17: 15 – 21* 18. (Abrahamu alitaka Mungu afanye kulingana na akili zake zilivyokuwa zimepanga!!**

2. Naamani karibu kabisa akose muujiza wake sababu ya kile alichokuwa anafikiri akilini mwake kwamba mtumishi wa Mungu Elisha angetakiwa kukifanya kwake kwanza (**2Wafal. 5: 11 – 12**). Ndani ya akili ya Naamani alifikiri kwamba kwa kuwa yeye ni mtu Mkuu anavyotetemekewa akifika mahali). Alijua nabii kwanza atatoka ili amlaki; halafu asimame aanze kumwombea, na kisha apitishie mikono yake katika sehemu zote za mwili wake zilizo na ukoma ndipo apone!!! Halafu pili akalinganisha maji ya mto

Jordani ambayo ni machafu akilinganisha na mito ya kwao!! Akaondoka kwa hasira.

- Kama asingepata washauri wema; kweli kabisa muujiza wake ulishoota mbawa sababu ya kwenda kwa Mungu wakati tayari akilini mwake amepanga nini Mungu akifanye kwake. Hata Yusufu alijaribiwa sana saa Yakobo anawabariki wajukuu zake (watoto wa Yusufu). **Mwanz. 48: 8 – 22.**

- **Sasa akina Naamani ni wangapi leo katika kanisa!!!** Watu ambao wanataka kujua Mungu anataka wafanye nini na midomo yao kuonekana wako tayari kufanya kile ambacho Mungu atawaambia wafanye lakini akilini mwao wana mipango yao ambayo wamepanga tayari kuifanya!!! **Yer. 42: 1-22, Yer. 43: 1-7.** Na wakati wote watu ambao wanataka wafuate akili zao zisizofaa, Mungu anawaacha ili waendeleo kufanya yasiyofaa na kuumia baadae. **Rum. 1: 28 – 32.** Soma **pia 1Wafal. 22: 1 – 28, 34 - 37. Na Kor. 1: 19 (Isaya 29: 13 – 14)**

3. Kuna faida kubwa sana katika changamoto tunazokutana nazo na ambazo zimetuchosha sana pale tunapotii na kufuata maelekezo ya Watumishi wa Mungu wanayotupa. **Luk. 5: 1 – 11.** Pamoja na Petro kuwa na uzoefu wa miaka mingi wa kuvua samaki na anajua samaki daima wanatembea kwa makundi usiku, na ukitaka uwanase katika nyavu lazima uvue usiku; lakini Yesu aliposema Petro alitii na kutweka hata kilindini; akaacha akili zake na ujuzi wake pembeni na kutii sauti ya Yesu na matokeo yake ni kupata samaki wengi mchana paupe kiasi cha nyavu zao kushindwa kubeba wingi wa samaki hizo!!!

- **Mojawapo ya sifa iliyomfanya Petro ainuliwe mno na Bwana Yesu ni ile hali yake ya kutii kila ambacho Bwana Yesu anamwambia afanye hata kama kwa akili zake hajawahi kabisa kujaribu kufanya kitu hicho. Math. 17: 24 – 27**

- **Agizo hili ni gumu sana kwa mtu anayetumia akili zake!! Mst. 27.**

- Lakini pia **Math. 14: 27 – 29:** Petro mvuvi maisha yake yote, anaambiwa tembea juu ya maji kwa miguu unifuata!!! Na anashuka na kutembea juu ya maji!!! Kwa vyovyote vile akili zake na ujuzi wake aliviweka kando pale alipoamua

kumwendea Yesu kwa miguu juu ya maji na kuwaacha wenzie wote (11) ndani ya mtumbwi!!!

- **Shida yetu kubwa sana leo ni ile hali ya kukaa katika wokovu, lakini tunatumia akili zetu mno katika kupata ufumbuzi wa matatizo yetu mengi.**
- **Soma tofauti ya Lutu na Abrahamu. Mwnz. 13: 8 – 18.**
- Kama mteule anajua cha kufanya katika akili zake (ufahamu wake) hata Mungu aseme naye/watumishi waseme naye atawasikiliza tu bila kuwaelewa na anabakia na msimamo wake ule ule kama jemadari Naamani!!! Ujuzi na akili zimeponza wengi na kuwaletea madhara baadae kama ilivyokuwa kwa Lutu pia.

“Siri” – Mungu akisema jambo, hata kama akili zako/ zangu zinakataa na kugoma na kuona kuwa hilo haliwezekani. **2Wafal. 7: 1 – 2;** wewe **zilazimishe zitii** tu hilo alilosema Mungu/Mtumishi wake ndipo utakaposhuhudia matendo makuu ya Mungu katika maisha yako kuliko kuendekeza akili zako ambazo zina mipaka katika baadhi ya mambo ya Mungu. Na kama kweli tunataka tutoke katika changamoto tulizonazo leo; lazima tu tukubaliane na kile anachokisema Mungu/watumishi wake na tutende kama wanavyotuelekeza.

2Nyak. 20: 14 – 30. Mfalme Yehoshafati alipoweka Kando ujuzi wake na uwezo wake na kufanya kama Mtumishi wa Mungu alivyoelekeza; mafanikio yakawa makubwa sana na ufalme wake ukatulia. **Amina.**

Na

Askofu Dr. L. M.Mwizarubi

March 2021